Uvuvi >> Kuwa nyenzo ya kuondoa umasikini, kuvutia uwekezaji na kuchangia uwepo wa m




NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Miaka 40 ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) sambamba na kuzindua mfumo maalum wa upatikanaji wa taarifa sahihi za uvuvi. Pia Dk. Biteko alishuhudia utiaji saini wa makubaliano ya TAFIRI na ZAFIRI kwenye mazao ya bahari, jijini Dar es Salaam, jana. (Picha na Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu).

# Mageuzi makubwa yaja sekta ya uvuvi

Dar es Salaam
**NA HAMIS SHIMYE**

MAGEUZI makubwa sekta ya uvuvi. Ndivyo unavyoweza sema baada ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko kueleza mipango mikakati ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Hali hiyo inatokana na serikali kutangaza kufanya kila liwezalo kuhakikisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) inafanya shughuli zake kwa ufasaha kuongeza tija katika Sekta ya Uvuvi nchini.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya miaka 40 ya taasisi ya TAFIRI ameitaka taasisi hiyo kuweka mkazo zaidi katika utafiti wa uvuvi katika Ukanda wa Bahari ya Hindi kwa kuwa bado mchango wake ni mdogo tofauti na mchango wa sekta hiyo upande wa maziwa.

"TAFIRI mchango wake uongezeke katika uvuvi wa Bahari Kuu ambapo bado mchango wake ni mdogo. Hakikisheni wizara na TAFIRI mnakuwa kimbilio la wavuvi muone fahari wavuvi wanakuwa matajiri." alisema

Dk. Biteko alisema Sekta ya Uvuvi kuwa nyenzo ya kuondoa umasikini na kuvutia uwekezaji pamoja na kuchangia uwepo wa mazao ya uvuvi nje ya nchi.

ULEGA AFUNGUKA

Kwa upande wake Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema wizara imeweka mkakati kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 Sekta ya Uvuvi ichangie katika pato la taifa katriban kwa asilimia kumi tofauti na sasa ambapo inachangia kwa asilimia 1.7 pekee.

Aliongeza kuwa wizara inalenga kuweka mazingira mazuri na kuratibu ufugaji samaki kwa wingi ili kuzalisha zaidi kutoka tani laki tano kwa sasa hadi tani laki sita ifikapo mwaka 2025/2026.

Alisema ufugaji wa samaki ni kipaumbele kwa wizara na kwamba TAFIRI imesaidia kuondoa baadhi ya vikwazo vya ufugaji wa kwenye vizimba katika Ziwa Victoria kwa kufanya tafiti ya maeneo ya ziwa hilo ambayo yanafaa kwa ufugaji.

Naye, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TAFIRI, Yahya Mgawe, ameiomba serikali kupitia kwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Biteko kununua meli ya utafiti yenye thamani ya Shilingi Bilioni 6 ili kusaidia kurahisisha shughuli za utafiti katika Ukanda wa Bahari ya Hindi.

Hivyo, alisema meli hiyo itasaidia pia kukuza Uchumi wa Buluu kwa kuainisha masuala mbalimbali yatakayochochea Sekta ya Uvuvi kukua zaidi.

CamScanner

Mkuu wa Tisa wa Wadau wa Lishe nchini.

"Fanyeni ufuatiliaji wa karibu na kutoa taarifa za utekelezaji mara

Aliomba wadau wa maendeleo waunge mkono juhudi hizo ili kuwezesha mashine hizo kuzalishwa kwa wingi kutumika katika maeneo

kirefu nchi imekuwa ikikabili changamoto ya upatikanaji wa vifaa vya kuchanganyia virutubisho kwenye vyakula.

minifu kwa kubadilisha vipuri halisi na vipuri feki.

HABARI LEO UK 4

# Biteko ataka sekta ya uvuvi iondoe umasikini

Na Mwandishi Maalumu

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk Doto Biteko ameagiza watendaji wa sekta ya uvuvi wafanye sekta hiyo kuwa nyenzo muhimu ya kuondoa umasikini.

Dk Biteko ametoa agizo hilo Dar es Salaam jana wakati wa maadhimisho ya miaka 40 ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (Tafiri) na kuzindua mfumo wa upatikanaji wa taarifa sahihi za uvuvi.

Pia alishuhudia kusainiwa makubaliano ya Tafiri na Zafiri kwenye mazao ya bahari.

"Hakikisheni Wizara pamoja na Tafiri mnakuwa kimbilio la wavuvi wakiwaona ninyi wajue majibu ya maswali yao watayapata kwenu, na muone fahari ya kuwaona wavuvi wanakuwa matajiri," alisema Dk Biteko.

Ameiagiza Tafiri iongeze mchango wa mauzo ya bidhaa nje ya nchi ili kuleta fedha zaidi za kigeni.

Dk Biteko alisema mauzo ya bidhaa yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 168 mwaka uliopita hadi kufikia Dola za Marekani milioni 249.



HABARI LEO UK 8.

# * Waliovamia ardhi taasisi ya utafiti wa mifugo waonywa *

**Na Amina Omari, Tanga**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imewataka wananchi waliovamia kwenye eneo la ardhi la Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (Taliri), Kituo cha Tanga kuhama katika eneo hilo ili kupisha miradi ya kitafiti inayofanywa na taasisi hiyo.

Wakazi hao ambao awali walifanya uvamizi katika eneo hilo kwa asilimia 51 wataendelea kubaki, lakini wale waliovamia eneo hilo kwa asilimia 48.6 watalazimika kupisha eneo la taasisi hiyo.

Hayo yalibainishwa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Daniel Mushi wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuhitimisha majadiliano baina ya viongozi wa wananchi waliopo kwenye maeneo hayo ya uvamizi.

Alisema wamekubaliana kuzingatia sheria na taratibu za kisheria zilizopo za umiliki wa ardhi ili kuepusha changamoto ya uvamizi kama hiyo na kusababisha uwepo wa migogoro isiyo ya lazima.

"Shamba lililovamiwa ni la taasisi ya serikali licha ya kwamba wananchi hao wote walitakiwa kuhama lakini busara za viongozi wa serikali wameelekeza wananchi waliovamia eneo kubwa kuachwa, wale waliovamia eneo la pili lakini ni wachache kupisha eneo hilo," alisema.

Alisema kupishwa kwa eneo hilo kutasaidia taasisi kuendelea na majukumu yake yaliyokusudiwa ikiwemo kuleta tija ikiwamo utekelezaji wa Mradi wa Kituo Atamizi cha vijana ili waweze kujifunza stadi za biashara kupitia mifugo na kujiajiri.

Aidha, alisema utekelezaji wa ujenzi wa kituo hicho utaanza baada ya kuwasiliana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili waweze kubaini maeneo ambayo yatachukuliwa na Taliri huku wananchi wakitafutiwa maeneo mengine waendelee na shughuli zao za kiuchumi.

Hata hivyo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba alisema baada ya makubaliano waliyoyafikia sasa mgogoro huo umekwisha na wananchi waliovamia wataweza kutafutiwa maeneo mengine.

"Tunashukuru sasa mgogoro huu umekwisha kwa makubaliano ya maridhiano na sasa taasisi itabaki kwenye eneo lake na wananchi waliovamia watatafutiwa maeneo mengine ya kuendeleza shughuli zao," alisema.

Hata hivyo, wananchi waliovamia waliiomba serikali kulinda maeneo yake kwa kuweka mipaka, badala ya kuyatelekeza na kusababisha vurugu ya uvamizi wa maeneo.

CS CamScanner